**Learning by Ear - Illiteracy**

**“A GIRL FINISHING SCHOOL”**

**Episode 05:** *"Kufaulu au la..."*

**Author:** Frédéric GAKPARA

**Editor**: Yann Durand

**Translator:** Anne Thomas

**Characters:**

**Latifa** *(Ana umri wa miaka 15. Ni binti yao Papa Wali na Mamoua. Mwaka wa tisa huu anaosoma. Ni mwerevu kiasi kwamba hajawahi kurudia darasa lolote. Hata hivyo anakabiliwa na tatizo la wazazi wake kutaka kumwachisha masomo wakati anapojiandaa kufanya mtihani.)*

**Teacher** *(Mwanamume mwenye umri wa miaka 36, mwalimu katika shule ya kina Latifa, anampenda sana Latifa kwasababu ya werevu wake na matokeo yake mema shuleni)*

**Zakia** *(Ana umri wa miaka 20, ni msichana aliye na uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki yake Latifa na ameajiriwa katika afisi ya wakala wa Utalii kutokana na tajriba yake ya kimasomo. Ni msichana aliyebahatika kutembelea mahali pengi na hukutana na watu wengi kazini mwake.)*

**Epiphane** *(Mvulana wa umri wa miaka 18, ameajiriwa na Papa Wali. Ni mwerevu sana lakini hawezi kusoma wala kuandika kwa kuwa hakupata fursa ya kujiunga na shule. Kadiri anavyopata shida kutoka na hali yake hiyo ya kutojua kusoma, ndivyo hamu yake ya kujua kusoma na kuandika inavyozidi.)*

**INTRO**

**Hujambo na karibuni kwenye kipindi cha Noa Bongo-Jenga Maisha Yako tukiwa katika sehemu ya tano ya mfululizo wa "Mtoto wa kike ahitimu"makala inayoelezea elimu na kutojua kusoma na kuandika.**

*Hali imekuwa ni ya kutatanisha nyumbani kwa Papa Wali tangu Latifa aliporejea shuleni.Mawasiliano kati ya Latifa aliye na umri wa miaka 15, na wazazi wake si mazuri.Kwa sasa hawamtii shughuli. Hali inatatizwa zaidi na matatizo ya fedha yanayomzonga mamake kwasababu ya kuchelewa kuulipa mkopo aliopewa na shirika la kufadhili biashara ndogo. Kwa hali hiyo Mamoua amegeuka kuwa mtu wa kukasirika kwa urahisi. Papa Wali naye muda mwingi hayupo nyumbani. Baada ya ratiba ya siku ya masomo kukamilika, Latifa amebaki na mwalimu wake kwa mashauriano kidogo. Jiunge nasi usikilize sehemu ya tano iitwayo**: kufaulu au la...***

**Scene 1, AT LATIFA'S SCHOOL**

Latifa na mwalimu

1. **ATMO: NOISE OF SCHOOLYARD – TRAFFIC**

2. **Teacher:** Sijui nini kinachoendelea, Latifa. Alama zako zimeshuka sana.

3. **Latifa:** (**Silence**) …

4. **Teacher:** Huna la kusema?

5. **Latifa:** (**Silence**) …

6. **Teacher:** Wenzangu wameniambia umekuwa ukijitenga na watu nami nimelishuhudia pia hilo unapokuwa darasani mwangu. Bila shaka una sababu ya kuwa hivyo!

7. **Latifa:** (**Silence**) …

8. **Teacher:** Kwani una mvulana unayempenda?

9. **Latifa:** Hapana, Mwalimu!!!

10. **Teacher:** Basi, una nini?

11. **Latifa:** Sijui, Mwalimu... (**Brief silence**) Siwezi kumakinika ninapofanya kazi zangu za shule.

12. **Teacher:** Kipi hasa kinachokusumbua hata ukose kumakinika ?

13. **Latifa:** (**Silence.**) Hali ya mambo nyumbani haipendezi, Mwalimu. Wazazi wangu hawanisemeshi. Nadhani nilikosea kuamua kurudi shuleni hata baada ya wao kuamua nikatize masomo yangu.

14. **Teacher:** Unadhani hivyo? Hatma yako ingekuwaje lau ungekubaliana na uamuzi wao?

**15.Latifa:** Wanakabiliwa na matatizo mengi ya kifedha, Mwalimu. Nami hapa nafikiria tu masomo yangu. Sikutenda haki. **(On the verge on tears).**

**16.Teacher:** Latifa, unavyofanya haina maana kwamba hujamtendea haki mtu. Ulichukua hatua inayofaa.

**17.Latifa:** Lau kama nilitenda haki, ningemkabidhi baba yangu fedha nilizolipia karo ili amalize matatizo yake...

**18.Teacher:** Masomo yako pia ni miongoni mwa matatizo yake. Hilo ndilo tatizo muhimu zaidi kwake.

**19.Latifa:** Basi kwa nini hanisemeshi? Huelewi hali ya mambo, Mwalimu! Wananichukulia kuwa mimi ndiye mkosa. Mimi ndiye niliyesababisha matatizo yaliyo nyumbani kwetu...

**20.Teacher:** Latifa, Ninakuhakikishia kwamba wewe siye sababu ya matatizo ya nyumbani kwenu. Huenda babako anahangaishwa na uamuzi wake na hivyo ameudhika au anashughulishwa na matatizo yake. Pengine amekasirika kwa kuwa ameshindwa kusimamia vyema biashara yake. Vyovyote vile, wewe hulaumiki.

**21.Latifa:** Iwe iwavyo na mimi pia ninahusika!

**22.Teacher:** Latifa, matatizo ya babako yanaweza kutatuliwa leo au kesho. Lakini ukichezea masomo yako leo hii, hutaweza kuyapata tena siku za usoni.

**23.Latifa:** Lakini siwezi kumakinika nyumbani ambako watu wote utadhani wamefiliwa; na mama naye siku haipiti bila kumtukana rafiki yangu wa dhati, ambaye kusema kweli ndiye anayegharamia elimu yangu!

**24.Teacher:** Inakubidi ujichangamshe. Hata kama hakuna unayemwona katabasamu, jaribu kuwa katika hali ya kuchangamka. Bila masomo, una mambo mawili, Latifa: ama utabahatika kupata kazi kwenye kampuni nzuri au huenda ukabahatika ukaolewa, au uishie maisha ya dhiki katika eneo fulani, jambo ambalo ni fedheha.

Elimu itakusaidia kwa kiasi kikubwa kujiimarisha kijamii na kisaikolojia. Hata unapokumbana na umasikini wa mali, uwezo wako wa kiakili utakusaidia katika hali nyingi. Nadhani unafahamu ninalokusudia?

**25.Latifa:** Ndiyo, Mwalimu!

**26.Teacher:** Wewe ni mtoto wa kike, Latifa, masomo ndiyo unayohitaji zaidi. Mwanamke siku hizi hawezi kuutegemea urembo wake. Kwa hivyo zingatia hayo. Ni mwezi mmoja tu umesalia kabla ya mitihani, ukishika mengine utatatizika. Umenifahamu?

**27.Latifa:** Ninafahamu, Mwalimu!

**28.Teacher:** Basi fanya bidii! Ninataka uwe makini zaidi, Latifa!

**29.Latifa:** (**Smiling**) Haya, Mwalimu! Ninakuahidi nitafanya hivyo!

**30.Teacher:** (**Smiling**) Sawa. Kila la heri!

**31.Latifa:** Na wewe pia, Mwalimu! Tutaonana kesho!

**32.Teacher:** Naam, tutaonana kesho!

## MUSIC

**33.NARRATOR:** *Mwanafunzi wetu ametiwa moyo na yuko tayari kuzikabili tena changamoto za masomo yake. Siku inayofuata Zakia, rafiki yake Latifa anamwalika Ephipane, mfanyikazi wa Papa Wali kwa chakula cha mchana kwenye mkahawa wa kazini kwao akitaka kujua jinsi anavyoendelea na masomo yake. Amekuwa akihudhuria madarasa kwa muda wa kiasi wiki tatu zilizopita.*

## <u>Scene 2, AT THE CANTEEN IN ZAKIA'S AGENCY</u>

Zakia na Epiphane

**34.ATMO: CANTEEN NOISE – BLURRED CONVERSATIONS – SOUND OF CUTLERY**

**35.Zakia:** Epiphane, mambo yanaendeleaje kwenye madarasa yako ya jioni?

**36.Epiphane:** Hali ni tulivu. Kila mtu anafunzwa kulinganana uwezo na ufahamu wake. Wanatumia muda mwingi tu kufahamisha mambo na ni wavumilivu. Kusema kweli hali ni nzuri.

**37.Zakia:** Na jambo gani muhimu zaidi ambalo umejifunza mpaka sasa?

**38.Epiphane:** Ninajua kuandika jina langu sasa...

**39.Zakia:** Alaa, kweli? Basi vizuri!

**40.Epiphane:** Ninajua sasa kutia sahihi…?

**41.Zakia:** Kwani hukuwa na saini hapo awali?

**42.Epiphane:** (**A bit embarrassed**) Eeehe … hapana dadangu… sikuweza kutia saini...

**43. Zakia:** Hilo si jambo la kukutia aibu, Epiphane. Sasa unawajibika na unajitahidi kufidia muda uliopotea.

**44. Epiphane:** Asante sana, dadangu. Singeipata fursa hii bila wewe.

**45. Zakia:** Shukran zote ni kwa Bwana na Bibi Hendrik. Huo ni mradi wao kwa kweli. Niliwatembeza kama sehemu ya majukumu yangu ya kazi. Papa Wali anaendeleaje?

**46. Epiphane:** Hana neno, dadangu.

**47. Zakia:** Mpaka sasa amekataa kujiunga na masomo ya jioni?

**48. Epiphane:** Mwajiri wangu? Hafuati ushauri wa mtu. Anashughulishwa tu na fedha.

**49. Zakia:** Je anatumia vifaa alivyopata kutoka kwa Wakfu wa Hendrik?

**50. Epiphane:** Hata! Amevifungia kwenye kabati! Mara kwa mara anasema amekuwa akifanya kazi hiyo kwa zaidi ya miaka 30 na kwamba cheche na miale ya “x-ray” havitamwangamiza sasa.

**51. Zakia:** (**She shouts to the waiter**) Ningependa kulipa, tafadhali!(**To Epiphane**) Huyo bwana haelewi lolote! Niliwapeleka Bwana na Bibi kwenye karakana yenu ili waweze kumsaidia atatue matatizo yake.

**52. Epiphane:** Mimi huvaa vitu vyote, dadangu! Glavu, kofia na magwanda ya ngozi... Kila kitu!

**53. Zakia:** Vizuri hivyo, Epiphane! Hali yako itazidi kuimarika ukiendelea hivyo. Na ni hivi karibuni!

**54. Epiphane:** Asante sana dadangu! Sitakuvunja moyo!

**55.SFX: SOUND OF COINS BEING COUNTED AND PUT ON THE TABLE**

**56. Zakia:** Sawa, nimesharejeshewa baki ya fedha zangu. Twen'zetu. Nina kazi chungu nzima inayonisubiri!

**57.SFX: NOISE OF CHAIRS**

**58. Epiphane:** Asante sana dadangu!

**59. Zakia:** Si neno, Epiphane! Kwaheri!

**60. Epiphanie:** Kwaheri!

**61.SFX: STEPS GOING AWAY**

## MUSIC

**62. NARRATOR:** *Siku kadhaa zinazofuata, Zakia anajitahidi kumchangamsha rafiki yake wa dhati kabla yake yeye kufanya mtihani. Aidha amewarejesha Bwana na Bibi Hendrik kwenye karakana ya Papa Wali wanunue samani za vyuma ili waipiga jeki biashara ya Papa Wali ndipo achangamke na akome kumtatiza Latifa. Sasa Latifa ameshamaliza mtihani na amefaulu vizuri na amechangamka kweli akiwa kwa Zakia!*

**Scene 3, IN ZAKIA'S BEDROOM**

Zakia na Latifa

**63.ATMO:** **LOUD POP MUSIC – SOUND OF GLASSES, VOICES**

**64.Latifa:** (**Laughing**) Eeh, Zakia! Ninahisi kama kisunzi hivi!

**65. Zakia:** **(Laughing)** Kwa sababu gani, Latifa? Mwangaza au kinywaji?

**66. Latifa:** Una maana gani unaposema kinywaji? Hakileweshi! Bila shaka ni mwanga!

**67. Zakia:** Waonaje tukienda kwenye klabu?

**68. Latifa:** Sijawahi kwenda kwenye klabu !

**69. Zakia:** Najua hujawahi. Twende leo jioni! Tunahitaji kusherehekea matokeo mazuri yamtihani wako.Ni wakati wako huu kufurahi hasa baada ya kutatizika kwa muda wote huo, au siyo?

**70. Latifa:** Naam, lakini hayo yote siyawezi. Kama kucheza muziki tunaweza kuchezea hapa.

**71. Zakia:** Si sawa na kwenda klabu!

**72. Latifa:** Naona haya yanatosha kwa kweli,Zakia. Tayari wewe umeshatimia umri wa miaka 20. Wazazi wako wanakuamini. Mimi na wewe hatuko sawa!

**73. Zakia:** Usijali!

**74.SFX:** **GLASSES BEING REFILLED**

**75.Latifa:** (**Laughing**) Basi usiijaze glasi, asante, Zakia!

**76. Zakia:** Nimefurahi sana kwamba umepita mtihani wako.

**77. Latifa:** Hali ilikuwa ngumu si kidogo!

**78. Zakia:** Ninajua; ndio maana mafanikio haya ni jambo la maana sana. Changamka Latifa, tufurahie ushindi wako. (**Shouting**) Ushindi ni wetu!

**79.SFX:** **GLASSES CLINKING TOGETHER**

**80.Latifa:** Ushindi ni wetu!

**81.SFX:** **MOBILE PHONE RINGING**

**82. Zakia:** (**Very happy**) Bila shaka huyo ni kakako! Nina hakika! (**She answers**) Hallo, Elinam? (…) (**Angrily**) Nani amekupa hii namba ya simu? (…) Unasemaje? (…) Usiwahi tena kupiga nambari hii ya simu! Sitaki uhusiano wako– si leo wala kesho. Koma kunisumbua au nitawaarifu polisi! (**Hangs up**) Watu wengine hawana adabu!

**83.Latifa**: Vipi! Zak! Ni nani huyo?

**84.Zakia**: Mwendawazimu! Huyu bwana amekuwa akinisumbua nje ya afisi yetu, ninapokataa mambo yake, wajua huniambiaje? *"Si wazungu pekee walio na fedha."*

**85.Latifa**: Alaa, maana alikuona na watalii wa kigeni?

**86.Zakia**: Ndo hivyo! Ndivyo hawa watu wanavyonidhania. Wanafikiri mimi ni chambo cha kuwavutia na kuwashawishi watalii kukaa kwa muda mrefu zaidi.

**87.Latifa**: Hilo ndilo jambo ambalo silifurahii katika kazi yenu.

**88.Zakia:** Ndivyo mambo yalivyo kila mahali, Latifa. Pindi mwanamke anapofanikiwa, wanaume hufikiri ni kwasababu ya mwili wake. Sitaki kumtegemea mwanamume yeyote mimi. Ninataka kujitegemea kufuatana na uwezo wangu na nitaendelea kujifunza ili niendelee kupanda ngazi kazini kwetu.

**89.Latifa:** Kweli hayo Zak! Inatubidi tusome, tujifunze na tujiandalie fursa zetu wenyewe. Lakini tusiyazingatie hayo sasa hivi. Tusiharibu sherehe yetu.Tucheze muziki!

**(They turn up the music, tease each other, shout and sing …)**

**OUTRO:**

*Marafiki wawili walicheza muziki mpaka usiku wa manane. La kushangaza ni kwamba, Papa Wali na Mamoua hawamkasirikii Latifa anapochelewa kurudi nyumbani . Fauka ya hayo Mamoua ingawa hampendi Zakia, anamwaga pale anapomsindikiza Latifa nyumbani. Kwa hivyo likizo ya Latifa inaanza katika hali nzuri ukiuzingatia uhusiano wake na Zakia. Lakini hali itadumu?Jee amani na maelewano yamerejea nyumbani kwa kina Latifa? Ili kufahamu zaidi, sikiliza sehemu itakayofuata ya* ***"Mtoto wa kike ahitimu****", makala inayoelezea masuala ya elimu na kutojua kusoma na kuandika.*

**Ukitaka kusikiliza kipindi hiki tena au vipindi vyengine vya NoaBongo – Jenga Maisha yako,tazama ukurasa wetu wa wavuti www.dw-world.de/lbe. Unaweza pia kutuandikia barua-pepe kupitia anwani:** lbe@dw-world.de
**Hadi wakati mwengine,kwaheri!**

**END OF 5th EPISODE**